

LEARNING BY EAR 2012

“Wasaliti walo karibu – Hadithi inayoangazia dhulma zinazoambatana na ngono”

EPISODE 2: ‘Mawindo na wawindaji’

AUTHOR: Chrispin Mwakideu

EDITOR: Andrea Schmidt, Pendo Paul

Proofreader: Pendo Paul

List of characters by scene:

SCENE ONE: ALLAN AND UNCLE JOE AT HOME

- Allan (m, 10)
- Joe (m, 45)
- Narrator (m/f, around 30)

SCENE TWO: NURU AT THE WATERHOLE

- Nuru (f, 30)
- Shoka (m, 50)
- Mixed male voices
- Narrator (m/f, around 30)

SCENE THREE: PATO SUMMONED BY MR. MANENO TO HIS OFFICE

- Pato (f, 16)

Noa bongo, jenga maisha yako 2012 – Wasaliti walo karibu – Ep. 2

- **Maneno (m, 45)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

SCENE FOUR: DULU VISITS JENA AT HER HOME

- **Dulu (m, 40)**
- **Jena (f, 25)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

UTANGULIZI:

Nakusalimu na karibu katika kipindi chetu cha redio **Noa bongo, jenga maisha yako**, hii ni hadithi mpya itwayo ‘**Wasaliti walo karibu**’ – mchezo unaoangazia dhuluma na unyanyasaji unaohusika na ngono barani Afrika. Katika kipindi chetu cha kwanza, Nuru rafikiye Jena aliachwa peke yake kisimani, na baadaye alijitupa ndani ya maji aliposikia dalili za waasi kumfikia. Ni nini kitakachojiri? Pia tulisikia kutoka kwa Pato, binti wa miaka 16 aliyejiunga na shule ya mabweni kwa mara ya kwanza. Halafu tulipata kumsikia Allan aliye na umri wa miaka kumi na mamake Precious ambaye alimtambulisha kwa ‘Uncle Joe’. Hawa wahusika wetu watatu watatupeleka wapi leo? Tutayang’amua haya yote katika kipindi hiki, kiitwacho ‘**Mawindo na wawindaji**’. Kwanza wacha tumsabahi bwana mdogo Allan, aliyeachwa nyumbani chini ya ulezi wa “Uncle Joe”.

SCENE ONE: ALLAN NA UNCLE JOE NYUMBANI

1. SFX: RADIO IN BACKGROUND, SPOON STIRRING SUGAR IN CUP

2. JOE: Allan, hiyo sukari ni nyingi mno. Kwani unatengeneza asali? Sukari nyingi si nzuri.

3. SFX: CLINK OF SPOON PUTTING IN MORE SUGAR

4. JOE: Wewe! Wacha kuharibu sukari! Nimesema imetosha, husikii wewe mtoto!

5. ALLAN: Hapa ni kwetu! Nitafanya chochote nitakacho.

6. JOE: Sikiliza, Allan, sijui mamako amekueleza nini. Lakini sitakubali huu upuuzi.

7. **ALLAN:** Basi ondoka! Kwani ni nani amekuzuia.

8. **JOE:** Chunga mdomo wako, Allan. Mimi si mamako.

9. **ALLAN:** **(shouts)** Na wala wewe si babangu!

10. **SFX: SLAP ON FACE**

11. **ALLAN:** **(screams in pain)** Aaaaah! Ondoka! Wewe si mjombangu! Kwenda! Sikupendi!

12. **JOE:** **(in fury)** Sawa! Nafikiri haijatosha! Nitakufunza adabu sasa hivi!

13. **SFX: TABLE AND CHAIRS BEING DRAGGED ASIDE**

14. **ALLAN:** **(trying to sound brave)** Subiri mamangu arudi! Nitakusemea...

15. **JOE:** **(stern warning)** Ati, thubutu! Ukijaribu, nitakukata masikio na ulimi wako. Unanielewa, Allan? **(shouts)** Umenielewa?

16. **SFX: SLAP ON FACE**

17. **ALLAN:** **(terrified)** Uncle Joe... pole, Uncle Joe. usiniumize, tafadhali. Sitamwambia mama, kweli. tafadhali...

18. **JOE:** Hebu kuja hapa. Mtoto mkorofi!

19. ALLAN: (screams out in fear) Aaaaah! Laaaa!! Tafadhali usinichape!

20. SFX: BEATINGS, SLAPS ETC

21. MSIMULIZI: Dhulma za kingono hufanywa aidha kimwili au kihisia, baada ya kitendo hicho, mdhulumiwa huhisi unyonge, huku mtendaji akijihisi mahiri. Ni kama simba anayesherehekea windo ambalo hakutoa jasho kuliwinda. Allan amedhulumiwa na mtu ambaye anastahili kuwa mlinzi wake. Atasubutu kumweleza mamake kweli, baada ya vitisho vya Uncle Joe? Jibu lake liko mumu humu kwenye kusikiliza. Kwa sasa, turudi kule kisimani, Nuru akiwa anatetemeshwa na waasi, wanaoongozwa na bwana Shoka, bado hawajamshuhudia alipo.

SCENE TWO: NURU KISIMANI

22. SFX : MIXED VOICES OF MEN LAUGHING AND THROWING BEER BOTTLES

23. NURU: (whispering) Oh Mungu wangu... isije ikawa wanakuja! Wanakuja huku! Oh Mungu – wataniua jamani...

24. SHOKA: (teasing) Yoohooo!!! Sasa bibiye... uko wapi, malikia... unamsubiri mpenzi wako huku? Sawa! Nimeshafika sasa... wasemaje? Wewe njoo upande gari letu, wanaume haya chap chap mtoeni

humo ndani.

25. SFX: HUGE LAUGHTER FROM MEN FOLLOWED BY GUNSHOTS

26. NURU: (trembling in fear) Wuuui – tafadhali msiniuee!!!!, msiniue!!! Nawaomba radhi. Tafadhalini niacheni niende – sijawakosea lolote.

27. SHOKA: Nani anataka kukuuu? Eh? Wanaume, hebu ingieni ndani mumtoe haraka.

28. SFX: FEET JUMPING INTO A POOL OF WATER

29. NURU: Tafadhalini msinijongeelee, usinikaribie! (**shouts**) Nisaidieni!!! Nisaidieni!!!

30. SHOKA: Hebu, kimya! Sitaki kusikia tena hizo nduru zako.

31. SFX: Nuru is gagged by piece of cloth as she continues to shout for help

32. SHOKA: Vyema. Sasa kama kiongozi wenu, lazima mimi nimuonje wa kwanza.

33. SFX: ONE SECOND OF SILENCE

34. MSIMULIZI: Hofu ya mwanamke yeyote – ni kunajisiwa. Na ni ndoto kushinda ya jinamizi kutendewa tendo hili na kundi la watu. Kuna matukio mengi, hadithi ni nyingi kwenye maeneo yenye rabsha ambako wanawake wengi wamekuwa wakiumizwa na hususan kunajisiwa. Sasa, maskini Nuru hakupona. Kama waathirika wote wa kingono, amejaaribu yote kujikinga. Haifai kumlaumu yeyote katika waathiriwa hawa kwani sio mapendeleo yao, na hakuna ajuae uchungu wa kiatu ila akivaae. Kwenye hali hii, Nuru alijaaribu awezavyo kujinasua lakini wapi. Alipiga kwata na mateke ili kuwafumua wanaume waliokuwa wanapishana zamu kumdhulumu na kumhujumu. Anajaribu kuyaokoa maisha yake na yale ya katoto kake kachanga kaliko tumboni. Lakini hatimae alisalimu amri. Kisha akahisi kana kwamba ulimwengu ulitanda giza: hakujua aliko wala aliyeko, wala masaibu haya yatakwisha muda gani. Hakujuwa pia kama waasi walishaondoka kwa gari lao. Nuru anavuja damu nyingi mno. Uchungu ulikithiri. Alijuwa wazi mauti yamemfika. Mawazo yake yalikuwa faraja... atafarijiwa na nani? Endelea kusikiliza upate ufahamu... lakini kwanza tuangazie yalioko kwenye shule ya mabweni, wakati Pato, alikuwa ameitwa ofisini kwa Mwalimu Mkuu, bwana Maneno.

SCENE THREE: PATO AKITAKIWA AFISINI MWA BWANA MANENO

35. SFX: KNOCK ON DOOR, FOOTSTEPS ENTERING

36. MANENO: Ingia...

37. PATO: Habari za jioni, Bw. Maneno. Uliniambia nije nikuone?

38. MANENO: (excited) Ah, mwanariadha wetu mchanga! Ndiyo - karibu, Pato. Ingia ndani, tafadhali rudisha mlango ukishaingia.

39. SFX: DOOR BEING CLOSED

40. MANENO: Vyema... Keti chini... hebu ketiii! Usiogope. Kwani umekosea nini.

41. PATO: Asante Bw. Maneno.

42. MANENO: Niambie, umependezwa na bweni unalolala? Umependelea kitanda chako? Namaanisha malazi yako?

43. PATO: (confused) Ee - ndiyo, mwalimu, nafurahi, asante sana.

44. MANENO: Umepata shida yeyote kutoka kwa mtu yeyote? Unajuwa, tunafahamu kuwa wanafunzi wa zamani hapa huwasumbuwa wale wageni.

45. PATO: La, hapana. Kwa sasa wote ni marafiki na wana ushirikiano mzuri nami.

46. MANENO: (insisting) Una hakika? Usimfiche mtu. Kumbuka, mimi niko hapa kuhakikisha makazi yako hapa ni salama.

47. **PATO:** Asante Bw. Maneno.

48. **SFX: CHAIR BEING PUSHED ASIDE**

49. **MANENO:** **(choosing his words carefully)** Na je kuhusu...
mmh... wavulana?

50. **PATO:** **(puzzled)** Hah?

51. **MANENO:** Wavulana humu shuleni. Hebu, Pato, nina hakika kuna wale waliokusumbuwa. Wewe u mgeni na isitoshe, ni mrembo, na... na... wapendeza.

52. **PATO:** Sikuelewi, mwalimu.

53. **MANENO:** Sawa. Tuwachane na hayo kwa sasa. Lakini kumbuka, kama kuna chochote wahitaji, usikose kuniuliza. Ni hayo tu.

54. **PATO:** Asante mwalimu, kwaheri mwalimu.

55. **SFX: FOOTSTEPS LEAVING**

56. **MANENO:** Oh – jambo jengine. Unaweza kuweka siri?

57. **PATO:** **(hesitant)** Naam... sidhani...

58. **MANENO:** Sio jambo kubwa, nimemwambia kiranja wa bweni lenu akupe godoro jipya. Lakini ni vyema ikiwa siri yako. Hiyo ni tunu – wanafunzi wachache hupata

magodoro mapya.

59. PATO: (a little puzzled) Ee ... asante, mwalimu...

60. SFX: DOOR BEING OPENED

61. MSIMULIZI: Inaweza kuwa ngumu kuamini, lakini Bw. Maneno ameanza kumvamia Pato. Kumbuka ana miaka 16 tu, na ni mwanafunzi. Yeye yuko kwenye nafasi ya kumuamuru; anastahili kumuongoza na kumuhusia. Kumpa kwake Pato tunu hizi, anajaribu kumtenganisha Pato na wasichana wengine. Kweli Pato ataweza kukwepa mtego huu? Lakini tukiacha nazi zigeuke mbata, hebu turudi kijijini, Dulu anamsubiri mkewe Nuru arudi kutoka kisimani alikokwenda kuchota maji. Wakati anapochelewa kurudi usiku unapoingia kweli ataingiwa na wasiwasi. Dulu anamwendea rafikiye Jena wanaokwenda wote kisimani kila wakati.

SCENE FOUR: DULU AMTEMBELEA JENA NYUMBANI KWAKE

62. ATMO: INSIDE THE HUT - EVENING VILLAGE ATMO OUTSIDE

63. JENA: (singing a lullaby)

64. SFX: BABY CRYING GENTLY

65. JENA: (sighs lovingly) Ah, huyu mtoto...nikubembeleze vipi, Chambo?

66. SFX: FOOTSTEPS APPROACH

- 67. DULU:** Habari za saa hizi, Jena.
- 68. JENA:** **(surprised)** Dulu! Umenishtua. Mbona hukunibishia?
- 69. DULU:** Pole. Sio nia yangu kukushtuwa. Namtafuta mke wangu Nuru.
- 70. JENA:** Nuru? Si.. si.. sikuelewi, kwani hajarudi nyumbani?
- 71. DULU:** La. Ndiyo maana niko hapa. Nyinyi si mlitoka wote asubuhi kwenda kuchota maji. Nikafikiri utajuwa alipo, nimemngoja tangu alipotoka, ndiyo sasa nikaingia wasiwasi.
- 72. JENA:** Kwa kweli, nilimu acha kisimani. Sijamuona tena mpaka sasa.
- 73. DULU:** **(bewildered)** Ati ulimuacha kule kisimani peke yake? Yeye tu? Kwanini? Si ilikuwa mwaterbea pamoja?
- 74. JENA:** Ndiyo, lakini mimi nilipitia kwa shangazi yangu mgonjwa. Lakini usijali, Dulu. Sidhani kama kuna jambo lolote baya. Labda amekwenda kumtembelea mtu.
- 75. DULU:** Hapana! Nina wasiwasi. Unajuwa ni mjamzito! Ninakwenda huko kumtafuta. Nuru si mtembeaji usiku. Hana tabia hiyo.

HITIMISHO:

Wakati Dulu anapojiandaa kwenda kisimani, nasi tunapiga fundu la maji katika kipindi hiki cha usomi kwa usikizi kwa isimu ya, '**Wasaliti walo karibu**'. Dulu atafanya nini akimpata mke wake katika hali ile? Kumbuka: Nuru amenajisiwa kinyama, na amelala majeruhi kando ya kisima. Na atatumia njama gani nyingine Bw. Maneno ili akapate kasichana kale ka miaka 16, Pato? Na Allan atamsimulia mamake kuhusu vamizi la Joe? Pata hayo katika kipindi kifuatacho.

Na ukumbuke, tunapenda sana kupata maoni yako. Tupatie kupitia tovuti yetu dw.de/lbe, au jiunge nasi kwenye mtandao wa Facebook. Mpaka tutakapokutana kipindi kijacho, kwaheri na baki Salama Salmin.